THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# SCHOOL BASED ASSESSMENT

# KISWAHILI
# SEHEMU B

**(For Regular Learners and Learners with Physical Disability)**

## Gredi ya 5 – 2024

**JINA LA MWANAFUNZI : ________________________GREDI :_______________**

**NAMBARI YA TATHMINI:_______________________________________________**

**TAREHE:_________________________________________________________________**

**JINA LA SHULE: ______________________________________________________**

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

**JEDWALI LA ALAMA**

| | ZOEZI : 3<br>UFAHAMU WA KUSOMA | ZOEZI : 4<br>SARUFI | ZOEZI : 5<br>KUANDIKA |
|---|---|---|---|
| Swali | 1-16 | 17-30 | 31 |
| Upeo | 16 | 14 | 10 |
| Alama za mwanafunzi | | | |
| Kiwango Cha Utendaji | | | |

**Tathmini hii ina kurasa 11 zilizopigwa chapa.**

**Geuza ukurasa**

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

## ZOEZI 3:UFAHAMU WA KUSOMA

**Swali la 1 hadi la 4**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*



Zainabu alifika darasani akiwa amechelewa kidogo. Mwalimu wa Kiswahili Bwana Busara alikuwa tayari ameingia darasani. Zainabu **alipiga hodi** na kusema,
"Samahani mwalimu nimechelewa. Ninaomba uniruhusu kuingia darasani."
Bwana Busara alimruhusu Zainabu kuingia kisha akaanza kufundisha.

Baada ya kipindi, Bwana Busara alimwomba Zainabu amfuate nje. Alimdadisi ili kujua sababu ya kuchelewa kwake. Zainabu alimweleza kuwa, walipokuwa wakitembea kuja shuleni, mdogo wake alijikwaa na kuumia. Ilibidi amshughulikie kwa kumpa huduma ya kwanza.

Bwana Busara alifurahishwa na kitendo hicho cha Zainabu. Alimpongeza na kumhimiza kuendelea kuwa na tabia hiyo. Bwana Busara alimwambia Zainabu arudi darasani. Zainabu alifurahi na kujiunga na wenzake darasani.

1. Zainabu alimkuta mwalimu wa somo gani darasani?

   ____________________________________________

2. Zainabu alitumia neno **samahani** kuonyesha:

   ____________________________________________

3. Unafikiri ni nini ambacho kingefanyinka kama Zainabu asingempa mdogo wake huduma ya kwanza?

   ____________________________________________

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

4. Eleza maana ya **piga hodi** kulingana na kifungu.

___

**Swali la 5 hadi la 8**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*



Kijiji cha Bidii kinasifika sana kwa kilimo cha ndizi. Karibu kila boma katika kijiji hiki lina migomba ya ndizi. Hata hivyo, Bwana Mbotela ndiye mkulima bora zaidi wa ndizi kijijini humo. Shamba lake zima limejaa migomba. Nayo imebeba mikungu kwa mikungu ya ndizi.

Watu wengi kijijini huvutiwa na jinsi migomba ya Bwana Mbotela ilivyonawiri. Muulize Bi. Chenza, mkewe Bwana Mbotela. Atakwambia kwamba hili ni tokeo la bidii na ushirikiano wao. Kila siku Bwana Mbotela na mkewe huamka alfajiri kabla ya jogoo wa kwanza kuwika na kuelekea shambani. Hapo, utawaona wameshughulika na kazi mbalimbali. Mara wananyunyizia migomba maji, mara wanaipalilia, mara wanavuna mikungu iliyokomaa. Nyakati kama hizi hawazungumzi sana. Pengine hutoleana neno moja moja tu la **kutiana moyo**. Hali huendelea hivyo hadi adhuhuri wanaporudi nyumbani kwa chakula cha mchana.

Bidii ya Bwana Mbotela na mkewe imezaa matunda. Si ajabu kuyaona malori yameegeshwa shambani humo yakipakiwa ndizi kupelekwa sokoni. Hali kadhalika, wanakijiji wenzao na hata majirani humiminika kwao kila uchao kupata maarifa kuhusu jinsi ya kukuza migomba. Hakika, Bwana Mbotela na mkewe in vielelezo vya kuigwa.

5. Kijiji cha Bidii kinasifika kwa:

___

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

6. Fikiria kwamba wewe ni jirani wa Bwana Mbotela na mkewe. Utajifunza nini kutoka kwao?

_______________________________________________

7. Bwana Mbotela na mkewe wakiuza ndizi wanapata pesa. Unadhani wanazitumia vipi pesa hizo?

_______________________________________________


8. Kulingana na kifungu, maana ya **kutiana moyo** ni:

_______________________________________________

**Swali la 9 hadi la 12**

*Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.*

( *Ni siku moja baada ya mashindano ya kukariri mashairi shuleni. Kadzo anakutana na mwalimu Bahati kwenye eneo la gwaride.*)



Kadzo: (*Akimtazama mwalimu.*) Shikamoo mwalimu!

Mwalimu: (*Akichangamka*) Marahaba, Kadzo. Habari za mchana?

Kadzo: Njema mwalimu.

Mwalimu: Hongera kwa kuibuka mshindi. Hakika shairi lako lilidhihirisha ubunifu mkubwa. Sote tulijifunza mengi.

Kadzo: Asante mwalimu ila huo ulikuwa ushindi wetu sote. Maelekezo yako yalinisaidia kuliboresha shairi langu. Kumbuka hata sikuwa na mada maalum. Wewe ndiye uliyenishauri nitunge shairi kuhusu maadili.

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

Mwalimu: Ndiyo nilikueleza lakini shairi lenyewe lilikuwa lako. Nilivutiwa na jinsi ulivyozingatia lugha ya ushairi. Hata vina na mizani ulizizingatia bila uelekezi wangu.

Kadzo: Ah! Mwalimu, unanisifu sana. Kumbuka hata wenzangu walisikiliza shairi langu hapo awali na kulitolea maoni. Kwa ufupi shairi nililowasilisha lilitokana na juhudi za wengi.

Mwalimu: Ni kweli Kadzo lakini hata uwasilishaji wako uliwavutia walimu na waamuzi ndiyo maana ukaibuka mshindi. Sisi tunaona kuwa ukiendelea hivi utakuwa malenga wa kutajika.

Kadzo: ( Kwa unyenyekevu) Asante mwalimu. Nitaendelea kujiimarisha.

Mwalimu: Karibu Kadzo.

Kadzo: Kwaheri mwalimu.

Mwalimu: Kwaheri ya kuonana.

9. Kadzo alikutana na mwalimu wake kwenye:
_______________________________________________

10. Nini kinaonyesha kwamba Mwalimu Bahati anawajali wanafunzi wake?

_______________________________________________

11. Kauli, hata wenzangu walisikiliza shairi langu hapo awali na kulitolea maoni imetumika katika kifungu. Kauli hii inaonyesha kwamba wanafunzi_______________

(walifurahia ushauri uliotolewa na mwalimu, walishirikiana katika ujifunzaji wao)

12. Unafikiri wanafunzi wengine walifanya nini baada ya ushindi wa Kadzo?

_______________________________________________

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

**Swali la 13 hadi la 16**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Zamani, ndege wote waiishi katika kijiji cha Pepea. Hata hivyo, hawakuwa na kiongozi. **Bila shaka unaweza kukisia kuhusu jinsi hali ya maisha yao ilivyokuwa.** Baada ya siku nyingi za fikra na kushauriana, waliamua kumchagua kiongozi. Wote walikubaliana kuwa Kasuku ndiye angesimamia uchaguzi huo.

"Asanteni sana ndugu zangu kwa heshima hii ila ninaona njia bora ya kudumisha haki ni **kuandaa** mashindano ya kupaa angani. Atakayekuwa wa kwanza kurudi ardhini ndiye atakayekuwa kiongozi wetu. Hivyo, uongozi utakuwa umetolewa kulingana na uwezo wala si sura, kimo au maoni yetu kumhusu." Kasuku alisema.

Siku ya siku ilifika. Ndege walijitoma uwanjani kwa matarajio makubwa. Mara Kasuku alipuliza kipenga. Anga ilijaa ndege wa kila aina. Kila mmoja anajitahidi kwa jino na ukucha kumpita mwenzake. Chini kule mashabiki walikuwa wakiwashangilia kwa sauti kuu. Kasuku aliwatazama ndege wenzake. Polepole alianza kuwaona wengine wakilegea, uchovu umewalemea. Alipomtazama Tai, alimwona akipaa kwa kasi ya umeme hadi juu karibu na mbingu.

Hatimaye safari ya kurejea chini ilianza. Tai aliongoza kwenye safari hiyo huku wengine wakimfuata kwa mbali. Alitua chini kwa utaratibu huku ndege wote wakimshangilia. Hapakuwa na jingine. Kasuku alichukua kipazasauti na kusema,

"Huyu ndiye kiongozi wetu."

13. Ndege waliishi katika kijiji cha ___________________.

14. Ni nini kinaonyesha kuwa ndege ni wenye hekima?

    ______________________________________________________________________

15. Kauli, **Bila shaka unaweza kukisia kuhusu jinsi hali ya maisha yao ilivyokuwa,** imetumiwa katika kifungu. Unafikiri hali ya maisha ya ndege ilikuwaje bila kiongozi?

    ______________________________________________________________________

16. Kulingana na kifungu, maana ya **kuandaa** ni _________________________________.

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

**ZOEZI 4: MATUMIZI YA LUGHA**

17. Amina alimsaidia Pili kubeba <u>tita</u> la kuni. Andika aina ya nomino iliyopigiwa mstari.

_______________________________________________

18. Katika kapu kuna maneno yafuatayo: jicho, nguo, funguo. Je, ni nomino ipi iliyo katika ngeli ya I-ZI?

19. Soma sentensi katika jedwali hili. Jaza nafasi.

| | |
|---|---|
| Mkoba mpya umenunuliwa leo. | Mikoba mipya imenunuliwa leo. |
| _____________________________________________. | Kuta zile zinapendeza. |

20. Chagua jibu sahihi.

    Baraka humheshimu nyanya. Nyanya humheshimu Baraka. Kwa hivyo?

    A. Baraka na nyanya huheshimiwa.

    B. Baraka na nyanya huheshimiana.

21. Wanafunzi **walipoketi** ukumbini, mgeni mwalikwa **alisimama** kuwapa ushauri.

    Alisimama ni kinyume cha aliketi.

    Tunga sentensi ukitumia kinyume cha neno, **enda**.

    __________________________________________________________________________

22. Geuza sentensi ifuatayo katika hali timilifu.

    Wanafunzi hushirikiana katika vikundi.

23. Kanusha sentensi hii:

    Mimi nilikariri shairi.

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

24. Tunga sentensi ukitumia ukubwa neno, **mji**.

_______________________________________________

25. Jaza pengo kwa alama ifaayo ya uakifishi.

Kwa nini Musa anatabasamu _____

26. Chagua chati yenye mfuatano sahihi wa maneno jinsi yanavyotokea katika Kamusi.

**A.**

i. meza
ii. meli
iii. methali

**B.**

i. hakika
ii. harusi
iii. hasara

**C.**

i. kipepeo
ii. kitanda
iii. kichana

27. Omari ni kaka ya mama yako. Je, wewe utamwitaje Omari?

_______________________________

28. Tunasema, Okelo ni mjanja kama sungura na Hamisi ni mpole kama_____________________________.

29. Jaza jedwali kwa kisawe kifaacho. Fuata mfano:

| | |
|---|---|
| mtu | mja |
| nyumbani | _______________________ |

30. Unamshauri rafiki yako awe na mazoea ya kutia bidii katika kazi zake. Chagua methali ambayo utatumia.

A. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

B. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

**ZOEZI 5 :KUANDIKA**

31. Andika insha yenye kichwa kifuatacho:

**SHEREHE YA KUVUTIA**

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*